# TAHARIRI

Elimu ni sekta muhimu katika nchi, wakubwa kwa wadogo wanategemea elimu ili waweze kutosheleza mahitaji ya maisha. Katika harakati za kutafuta elimu, kuna changamoto kadhaa ambazo zinarejesha nyuma upatikanaji wa elimu bora, kwa mfano: upungufu wa walimu, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani ubovu wa madarasa, uchache wa madarasa na vikalio, ukosefu wa miundombinu ya umeme na maji katika skuli pamoja na kutokuwepo kwa walimu maalum ambao watawasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kujifunza kwa wepesi

Elimu ni haki ya kila mtu, kwahivyo kila mmoja kwa nafasi yake hana budi kushirikiana na wenzake ili watoto waweze kupata haki hii ya msingi. Suala la ushauri nasaha ni muhimu kuwepo katika mazingira ya upatikanaji wa elimu ili kuwasaidia wanafunzi kuwa makini zaidi.

Matamasha na michezo mbalimbali huandaliwa katika skuli, hali ambayo inawasaidia wanafunzi kukusanyika na kubadilishana maarifa na ujuzi baina yao. Jambo hili huwafanya wanafunzi wawe wenye busara na hekima nyingi zitakazowasaidia katika maisha ya baadaye. Aidha, hali hii humpa mwanafunzi fursa ya kupumzisha akili baada ya kusoma kwa muda mrefu. Kawaida mwanafunzi hawezi kujifunza katika mazingira yasiyo rafiki, mazingira yenye utulivu na vifaa maalumu vya kufundishia vinahitajika kuwepo ili masomo yawe yenye mafanikio. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga skuli za kisasa zenye maabara na maktaba ili kupunguza wimbi kubwa la wanafunzi madarasani. Aidha, imeweza kusambaza vifaa kama vile vitabu, madaftari ya wanafunzi kwa skuli za msingi na sekondari, chaki na vifaa vya michezo.

Hali hii humwezesha mwalimu na mwanafunzi kushirikiana vyema katika tendo la kufundisha na kujifunza.

Hivyo, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi za kuimarisha elimu na kufanya bidii kuhakikisha changamoto inakabiliana nazo hususani zinazowahusu walimu ili kufanikisha maendeleo katika sekta ya elimu.

## YALIYOMO


- Tahariri.....UK.2
- ZATU na Siku ya Walimu Duniani.....UK. 3
- Risala ya Walimu katika Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani 05/10/2023 katika Ukumbi wa Benjamin William Mkapa, SUZA, Compus.....UK.4,5&6
- Dhana ya Afya na Usalama Kazini .....UK. 6,7,8,9 & 10
- ZATU yafanya uchaguzi wake .....UK.10 &11


## BODI YA UHARIRI


Daud M. Ali - M/Kiti

Tuvunao M. Jabiri - Katibu

### Wajumbe

Haji J. Omar

Mwanajuma H. Faki

Ikram M. Ali

Halima B. Mohamed

# ZATU NA SIKU YA WALIMU DUNIANI

Oktoba 5 ni Siku ya Walimu Duniani. Hapa Zanzibar, Siku ya Walimu ilianza kuadhimishwa mwaka 1979, chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Hata hivyo kufuatia kuanzishwa kwa ZATU mwaka 2002, maadhimisho hayo yalianza kuadhimishwa na ZATU kuanzia mwaka 2013.

Kwa mwaka 2023 tunapaswa kujipongeza kwa mafanikio yaliyopatikana. Pia, kujipanga kuzikabili changamoto zinazomkabili mwalimu na elimu kwa ujumla kwa mwaka ujao.

Walimu tumeshuhudia mafanikio mengi yatokanayo na Serikali ya Awamu ya Nane, kama vile, nyongeza za mishahara, kuthibitishwa kazi walimu, kuongezeka kwa posho la walimu wakuu na wasaidizi na kujengwa skuli nyingi za kisasa Unguja na Pemba.

Kwa Mwaka 2023 Maadhimisho hayo yamefanyika Pemba katika Ukumbi wa Benjamin William Mkapa, SUZA.
Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni Kuwepo kwa Tume ya Utumishi ya Walimu Zanzibar, Itasaidia Kutatua Changamoto Zinazowakabili Walimu wa Zanzibar

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar (WEMA) akifungua kongamano la Siku ya Walimu Duniani, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa WEMA alisema ni haki ya kila mwalimu kuhakikisha anapata stahiki zake. Pia WEMA imeihakikishia ZATU kushirikiana kwa pamoja katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika sekta hiyo.

Aliendelea kwa kusema kuwa,wapo baadhi ya walimu wakuu wameshindwa kusimamia majukumu yao ipasavyo, hivyo ni vyema kuhakikisha kila mmoja anawajibika katika majukumu yake. Aidha, Katibu Mkuu huyo amewaomba walimu ambao bado hawajajiunga na ZATU kuhakikisha wanajiunga ili waweze kutatuliwa kero zao kwa haraka.

Naye Afisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu Pemba Mwl. Mohd Nassor Salim amesema zaidi ya walimu 1446 wameajiriwa katika kisiwa cha Pemba Januari hadi Oktoba 2023, hivyo walimu wanapaswa kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi zaidi.

Aliendelea kusema kuwa matokeo ya kidato cha nne bado hayajaridhisha kwa mikoa yote Kaskazini na Kusini Pemba, hivyo ni jukumu la kila mmoja awajibike ipasavyo ili wanafunzi waweze kufanya vizuri zaidi.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar Mhe. Moh'd Said Dimwa ameitaka serikali kuhakikisha inafanya mchakato haraka wa kupatikana Tume ya Utumishi ya Walimu Zanzibar.




Naibu Katibu Mkuu CCM (wakatikati), Katibu Mkuu WEMA (wa kwanza kushoto), Afisa Mdhamini WEMA Pemba (wa pili kushoto) katika picha ya pamoja na viongozi wa ZATU.

## RISALA YA WALIMU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA WALIMU DUNIANI 05/10/2023 KATIKA UKUMBI WA BENJAMIN WILLIAM MKAPA (BMW) SUZA, COMPUS.

ZATU inaipongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada za kipekee za kuleta mageuzi ya elimu Zanzibar.

Miongoni mwa mambo ambayo walimu tunapongeza azma ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kukubali kuwa Walimu tupatiwe Tume ya Utumishi ya Walimu Zanzibar. Kupatikana kwa Tume ya utumishi ya walimu kutatatuwa kero nyingi za kiutumishi kama vile:

i. Likizo.
ii. Kupandishwa madaraja.
iii. Nyongeza za mishahara.
iv. Majukumu ya uongozi wa elimu kwa walimu.
v. Kupata chombo maalum cha kufanya majadiliano kama waajiriwa.
vi. Kuimarisha majadiliano kati ya vyama vya walimu na serikali kuhusu viwango vya mishahara na maslahi ya walimu.

Pamoja na pongezi hizi pia tunaiomba serikali izingatie muda wa masaa ya kazi kwa siku na kwa wiki kwa mwalimu kutokana na vipengele vifuatavyo

i. Idadi ya wanafunzi ambao mwalimu anatakiwa kuwahudumia kwa siku na kwa wiki. Licha ya jitihada zinazofanywa na serikali, bado kuna mazingira ambayo walimu wanabeba mzigo mkubwa wa wanafunzi pasina kuzingatiwa uwiano wa muda wa masaa ya kazi.

ii. Kupewa muda wa kutosha wa kupanga na kutayarisha masomo na kuwapima wanafunzi kutokana na masaa ya kazi. Suala la kupanga na kutayarisha masomo kwa walimu hayajapewa nafasi katika masaa ya kazi. Matokeo yake walimu hukosa muda muafaka wa kujitayarisha au kutumia muda wao wa nje ya masaa ya kazi kwa kupanga na kutayarisha masomo bila kuzingatiwa kwa kufanya kazi muda wa ziada.

iii. Mahitaji ya muda ambao mwalimu atashiriki kazi zilizo nje ya kufundisha ikiwemo kazi za kuwasimamia wanafunzi na kutoa ushauri nasaha.

iv. Muda ambao mwalimu atashauriana na wazazi juu ya maendeleo ya mwanafunzi.

v Walimu wanaopewa majukumu ya kusimamia pamoja na majukumu ya kufundisha, muda wa kufundisha upunguzwe kulingana na majukumu aliyopewa.

vi. Kwa mwalimu ambaye amezidi kiwango cha masaa yaliyowekwa apewe posho la ziada kwa masaa yaliyozidi kwa kiwango kilichokubaliwa.

Kutokana na kuwa walimu tunaamini kabisa kuwa uwalimu ni bahati. Kwa kujivunia ualimu wetu walimu tumekuwa tukifanya kazi kwa masaa ya ziada, kwa kuzingatia mapendekezo ya Umoja wa Mataifa kuhusu hadhi ya walimu. Ukizingatia masaa ya kufundisha ya mwalimu, mwalimu inabidi atumie muda akiwa nyumbani kufanya matayarisho ya somo, utayarishaji wa vifaa vya kufundishia, kupitia kazi za wanafunzi, pamoja na majukumu mengine ya uongozi wa skuli licha ya kuwa masaa hayo hayahesabiwi katika muda wa kazi. Tunaomba kupatiwa muongozo rasmi wa kuweka ukomo wa kazi za mwalimu na masaa anayotumia mwalimu katika kazi yake ili kuleta ufanisi zaidi.

**Katibu Mkuu ZATU aliendelea kueleza;**

Siku ya Walimu Duniani ni mahsusi kwa walimu kutathmini mafanikio na kujipongeza kwa yale tuliyoweza kuyafikia na kuzitafakari changamoto zinazotukabili na kuona namna ya kuzitafutia ufumbuzi.

ZATU inaamini kuwa mafanikio tuliyoyapata katika sekta ya elimu katika kipindi hiki ni makubwa na ya kupigiwa mfano. Sote tunashuhudia kwamba, Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi amepania katika kuimarisha huduma za jamii. Kwa dhati kabisa, ZATU tunakuomba utufikishie salamu na pongezi kwa mpendwa Rais wetu. Tuna faraja kuona kuwa uamuzi wake wa kuzipa kipaombele sekta zinazotoa huduma kwa jamii ikiwemo sekta ya elimu zimezidisha imani na mapenzi makubwa kwa jamii, tunachukua fursa hii kutoa nasaha kwa walimu na wananchi kuunga mkono jitihada za Mhe. Rais za kuleta mabadiliko chanya ya uchumi katika taifa letu.

**Katibu Mkuu aliendelea kueleza;**

Uanzishwaji wa majengo mapya ya ghorofa katika maeneo ya mjini na vijijini, ukarabati wa skuli zilizochakaa na ujenzi wa maabara mpya na za kisasa, umetoa sura mpya ya maendeleo ya elimu hapa Zanzibar. Aidha, kuajiriwa kwa walimu na kutoa kipaombele cha ajira kwa skuli tengefu kumedhamiria kusaidia kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa walimu. Jitihada hizi za serikali tunaziunga mkono, na sisi walimu tunasema tunajivunia uwalimu wetu kwenye malezi bora unayotulea wewe ni mwalimu mwenzetu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

**Katibu Mkuu aliendelea kueleza;**

Tunatambuwa jitihada zako Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuisimamia sekta ya elimu sisi Wanazatu tunakupongeza kwa uongozi wako thabiti katika sekta ya elimu na tunakuahidi kukuunga mkono ili kufikia azma ya serikali ya kutoa elimu bora kwa watoto wa Taifa letu. Tunathamini maono yako ambapo yamethibitisha kuwa wewe ni tiba ya matatizo ya elimu kwa Zanzibar. Kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita mwaka 2023, kumetokana na jitihada za walimu, wanafunzi, wazazi na wafanyakazi wote chini ya uongozi wako thabiti. Aidha, pongezi ulizozitoa kwa walimu kutokana na matokeo mazuri ya mitihani, zimewatia moyo walimu na kuona kweli mama yetu unatujali na kututhamini. ZATU inaamini kuwa utaendelea kutujali kwa kutusimamia tuweze kupata, stahiki mbali mbali kwa wakati ili hali za walimu zizidi kuimarika na mazingira mazuri ya ufundishaji katika skuli zetu.

**Katibu Mkuu aliendelea kueleza;**

Tunaamini kabisa kupitia uongozi huu thabiti, asilimia 25 ya posho la kufundishia, fedha za uendeshaji wa skuli, nyongeza za mishahara ya walimu na posho la walimu wakuu hayatakushinda kutokana na umahiri wa utendaji kazi wako. Tunaimani na wewe licha ya kuwa changamoto hizi zinatupa wakati mgumu katika utendaji wa kazi zetu hata hivyo, hatuvunjiki moyo.

**Katibu Mkuu aliendelea kueleza;**

Pamoja na yote hayo, ZATU inajivunia mahusiano mazuri na yanayozidi kuimarika siku hadi siku kati ya ZATU na Wizara ya Elimu. Mahusiano haya, yamesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za walimu ambazo zinapunguza ufanisi katika sekta ya elimu. ZATU tunaamini kuwa mahusiano mema na kuaminiana kukiimarika zaidi tunaweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kutatuwa changamoto nyingi kwa manufaa mapana ya taifa letu.

Hivyo, ZATU inaendelea kuwaomba walimu wote wajiunge pamoja ili kuwa na nguvu ya pamoja kama Mhe. Rais wa Zanzibar alivyoelekeza kuwa walimu wote wawe wanachama ili tupate kusikilizwa kwa urahisi.

**Katibu Mkuu aliendelea kueleza;**
Kwa wingi wa heshima natumia fursa hii kufikisha maombi ya walimu yaliyowasilishwa mbele ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa ZATU tarehe 12/02/2023, katika Ukumbi wa ZSSF Tibirinzi Pemba. Licha ya kuwa Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo bado hatujapata ufumbuzi wake.

**Maombi hayo ni kama yafuatayo:**
1. Nauli za walimu za kwenda na kurudi kazini kwa walimu ambao wanafundisha katika skuli za umbali unaozidi kilomita tano
2. Madeni ya nauli za walimu ambazo hazikulipwa wakati wa kipindi cha ugatuzi
3. Posho la ufiwa ambapo walimu wanalipwa chini ya kiwango kilichoekwa kwa mujibu wa toleo la serikali.
4. Uanzishwaji wa Tume ya Utumishi ya Walimu Zanzibar.



Katibu Mkuu ZATU akisoma risala ya walimu katika Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani 05/10/2023 Katika Ukumbi wa Benjamin William Mkapa (BWM), SUZA Compus.

## DHANA YA AFYA NA USALAMA KAZINI.

Afya na usalama kazini ina maana ya kulinda na kuendeleza afya ya mfanyakazi kimwili, kiakili na kijamii kwa wakati wote anapokuwa kazini. Elimu hiyo itamsaidia kuyatambua matatizo yanayotokana na kazi na jinsi ya kujikinga na ajali.

Afya na usalama mahali pa kazi ni suala mtambuka ambalo linagusa sekta za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na viwanda, ujenzi, kilimo, elimu, afya na maeneo mengine ya kazi.

Kazi ndiyo muhimili wa maisha ya mwanadamu. Wafanyakazi hutumia wastani wa masaa 8 kwa siku kwa kufanya kazi, iwe ni viwandani, ofisini na katika skuli n.k.
Kwa hivyo, mazingira ya kazi yanatakiwa yakidhi matakwa ya afya na usalama.

Suala la usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi ni jukumu ya kila mtu ili kupunguza mazingira hatarishi ya kazi.

### MIKATABA NA SHERIA MBALI MBALI ZINAZOHUSU AFYA NA USALAMA KAZINI.

Zipo sheria za kimataifa na kitaifa zinazohusu afya na usalama kazini. Shirika la Kazi Duniani limeainisha sheria zifuatazo:
- (Maazimio ya ILO 155, 161, 170)
- Kanuni ya 155 – inahusu utengenezaji wa SERA ya afya na usalama kazini
- Kanuni ya 161 – inahusu utoaji huduma ya afya na usalama kazini
- Kanuni ya 170 inahusu udhibiti na matumizi ya kemikali

Kila kazi ina mazingira yake na mengine huwa ni hatarishi kwa kiwango fulani kutokana na:

1. Mashine - Madhara yake ni kelele na ajali.

2. Mazingira ya nje (hewa, mwanga, mvua) - Madhara yake ni joto, vumbi, mionzi, mitetemo na unyevunyevu.
3. Mazingira ya kibaolojia (bacteria, virus, fungus) - Madhara yake ni kipindupindu, minyoo, homa, kichocho, fungus.
4. Kemikali / vimiminika - Madhara yake ni maradhi ya ngozi, ugumba, kuharibu mifumo ya hisia.

## AJALI NA MAGONJWA YATOKANAYO NA KAZI

Mamia ya wafanyakazi wameathirika kutokana na kazi zao bila kujua. Hali hii inatokana na kutopima afya mara kwa mara. Hali iliyopelekea wafanyakazi wengi Kupata matatizo yafuatayo:

- Maumivu makali ya kifua, mgongo n.k.
- Upofu wa macho.
- Ulemavu
- Magonjwa sugu
- Utasa au mimba kuharibika.
- Magonjwa ya kuharisha, homa, malaria n.k.

Kwa upande wa Zanzibar Sheria namba 8 ya mwaka 2005 ndiyo inayosimamia masuala ya afya na usalama kazini.
Kif. 4-5, 13, 18-19, 20

## Sheria hii ya afya na usalama kazini (Occupation Safety and Health(OSH)) inatekelezwa kwa:

## SHERIA YA AFYA NA USALAMA KAZINI

### Maeneo yanayozungumzia uongozi na utekelezaji wa sheria

a. Kusimamia kazi za Idara ya Usalama na Afya Kazini.
b. Kufanya na kusimamia ukaguzi wa usalama na afya katika maeneo ya kazi.
c. Kuweka na kudumisha rejista ya maeneo ya kazi.
d. Kutunza kumbukumbu na rejista nyingine za mambo mengine yoyote ambayo yanahitaji kusajiliwa chini ya sheria hii.
e. Kuweka kumbukumbu za uchapishaji kuhusu usalama na afya kulingana na viwango ambavyo vimejumuishwa katika kanuni.
f. Kuweka kumbukumbu za marekebisho au mabadiliko ya viwango vya afya vilivyochapishwa.
g. Kufanya kazi nyengine kama zitakavyohitajika chini ya sheria hii.

### 1. Njia za kumpata mwakilishi wa afya na usalama sehemu za kazi

a. Kuwe na wafanyakazi zaidi ya 10 katika sehemu ya kazi.
b. Sheria ya OSH itaanza kutumika ndani ya miezi 4 au kutoka wakati ambapo idadi ya wafanyakazi itazidi 10.
c. Mwajiri na wafanyakazi wataandaa mipango na taratibu zao wenyewe kuhusu muda wa ofisi kuteuwa au kuchagua mwakilishi wa afya na usalama kazini na iwapo itashidikana suala hilo litawasilishwa katika kamati ya afya na usalama kazini kwa usuluhishi na uamuzi.
d. Kila mfanyakazi alieajiriwa atastahiki kuteuliwa kuwa muwakilishi wa afya na usalama kazini katika sehemu hiyo ya kazi.
e. Shughuli zote zinazohusiana na uteuzi, kazi na mafunzo yatafanyika wakati wa saa za kazi za kawaida.

### 2. Majukumu ya mwakilishi wa afya na usalama kazini

Kazi za mwakilishi wa usalama na afya kazini alieteuliwa mahali pa kazi chini ya Sheria ya OSH No. 8 ya 2005 ni pamoja na -

a. Kukagua ufanisi wa hatua za afya na usalama.
b. Kutambua hatari zinazoweza kutokea na matukio makubwa mahali pa kazi.

c. Kushirikiana na mwajiri, kuchunguza sababu za matukio mahali pa kazi.

d. Kuchunguza malalamiko ya mfanyakazi yeyote yanayohusiana na afya au usalama wa wafanyakazi kazini.

e. Kukagua hati yoyote ambayo mwajiri anatakiwa kuweka kwa mujibu wa sheria ya OSH No.8 ya 2005 kwa kadri inavyowezekana ili mwajiri aweze kutekeleza majukumu yake.

f. Kuambatana na mkaguzi katika ukaguzi wowote.

g. Kushiriki katika ukaguzi wowote wa ndani wa afya au usalama.

h. Kuripoti ajali, vihatarishi vya majanga, majeraha, magonjwa, vifo na kutofuata maelekezo ya mkaguzi.

### 3. Wajibu wa mwajiri kuhusu usalama na afya kazini

Kif. 40 – 44, 58Kif. 84. kupima afya ya mwajiriwa,

(a) Usajili wa sehemu zote za kazi pamoja na mitambo na zana zinazotumika katika uzalishaji au kutoa huduma.

(b) Matumizi ya vifaa vya kinga za ajali na maradhi yanayotokana na ajira.

(c) Utoaji wa taarifa za ajali na maradhi yanayotokana na ajira.

(d) Kuundwa kwa chombo cha kusimamia afya na usalama.

(e) Ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu za kazi.

Sheria inataka majengo ya sehemu za kazi yawe madhubuti. Jengo liwe katika hali itayowalinda waajiriwa kutokana na:-

i. Hali ya hewa.   ii. Mapaa yasiyovuja.

iii. Unyevunyevu unaoweza kuliathiri jengo lenyewe au afya za wafanyakazi.

iv. Liwe katika hali ya kuwawezesha watu wenye mahitaji maalumu waweze kuingia kwa urahisi

Hatua zichukuliwe kuzuia waajiriwa kuathirika na kelele wanapokuwa kazini.

**Mwajiri anawajibu wa kuweka: -**

a. Maji ya kunywa yaliyo safi.

b. Vyoo vya kutosha kwa ajili ya waajiriwa na viwe safi pamoja na kuwa na taa, patenganishwe kati ya vyoo vya wanawake na wanaume na kwa wastani ila choo kimoja kihudumie si zaidi ya watu 25.

c. Vyombo vya kunawia kutegemeana na aina ya kazi.

d. Sehemu ya kutosha na inayofaa kuweka nguo ambazo hazivaliwi wakati wa kufanya kazi na sehemu hiyo itenganishwe baina ya wanaume na wanawake.

e. Kisanduku cha Huduma ya Kwanza kikiwa na vifaa vya huduma hiyo na kitunzwe na mtu aliyepata mafunzo ya Huduma ya Kwanza.

f. Usafiri wa uhakika wa kumfikisha hospitali mwajiriwa anapoumia na kuhitaji matibabu zaidi.

### HUDUMA YA KWANZA

Huduma ya Kwanza ni msaada unaotolewa kwa mfanyakazi aliepata ajali kama kuungua moto, kuanguka, kuangukiwa na kitu kizito, kuzama majini, kunaswa na umeme, kungongwana nyoka, kuumizwa na mitambo n.k kwa nia yakumpunguzia maumivu au kuokoa maisha yake. Ili kuweza kutoa Huduma ya Kwanza kwa ukamilifu, waajiri wanatakiwa kuajiri watoajiwa Huduma ya Kwanza watakaokuwepo mahalipa kazi wakati wote wa kazi.

### KISANDUKU CHA HUDUMA YA KWANZA

Kisanduku cha Huduma ya Kwanza kinatakiwa kuwa na vifaa vyote vinavyohitajika katika utoaji wa huduma yenyewe. Kwa kawaida Kisanduku cha Huduma ya Kwanza huwa na vyombo na vifaa vifuatavyo:-

Bandeji, aina mbali mbali za vitambaa vya kufungia vidonda, kitambaa safi kwa ajili ya kufungia jicho, bandeji ya pembe tatu, glavu na sabuni.

Kisanduku cha Huduma ya Kwanza lazima kiwepo mahali panapofikiwa kwa urahisi eneo la mahali pa kazi. Kisanduku cha Huduma ya Kwanza ni lazima kikaguliwe mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba kila kitu kinachohitajika kinakuwepo.

Kuwepo kwa vikalio kwa waajiriwa wanaosimama, kuondoa vumbi au moshi iwapo kazi inayofanywa inatoa vumbi au moshi au uchafu mwengine wa aina ya kiasi ambacho kinaweza kuleta madhara au kero kwa waajiriwa.

Endapo waajiriwa wanafanya kazi inayowafanya wawe karibu na kitu chochote chenye kudhuru au katika mazingira ya hatari muajiri anapaswa:-

Kuwapatia vifaa maalum vya kinga. Mfano:

- Kioo cha kukinga macho na uso, kinga za masikio, vichuja hewa, vichuja vumbi, barakoa, glavu, mabuti n.k

## HAKI NA WAJIBU WA WAAJIRIWA

Mwajiriwa anapokuwa kazini ana wajibu ufuatao:

(a). Kuchukua hadhari kwa usalama na afya yake binafsi na watu wengine ambao wanaweza kuathirika na utendaji wake wa kazi.

(b). Kushirikiana na wenzake kama inavyohitajika kuwezesha kutimiza wajibu au masharti wanayotakiwa kuyatimiza.

(c). Kuripoti hali ya hatari.

(d). Kutoharibu kwa makusudi au kwa uzembe kitu kilichowekwa kwa ajili ya afya, usalama au ustawi kutokana na masharti ya sheria hii. Kila penye wajibu pia pana haki.

**Mwajiriwa ana haki zifuatazo:**

(a). Haki ya kukimbia hatari. Mwajiriwa ana haki ya kuondoka sehemu ya kazi endapo anaamini kwamba hatari inaweza kutokea na kusababisha hasara kwa maisha au afya. Mwajiriwa huyo hatochukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa hatari hiyo itathibitishwa na Mkurugenzi.

b). Haki ya kutoadhibiwa kutokana na tendo lolote alilolifanya katika kutekeleza masharti ya sheria hii.

## MIKAKATI YA KUCHUKUA ILI KUBORESHA AFYA NA USALAMA KAZINI

- Hifadhi na matumizi bora ya vitendea kazi, mali ghafi na mazao.
- Kuboresha huduma muhimu za jamii sehemu za kazi mfano vyoo, migahawa, mahali pa kubadilishia nguo, vituo vya watoto na huduma ya maji.
- Kuimarisha usafi wa mazingira.
- Kuwepo na sera na sheria za afya na usalama kazini kwa sekta zote.
- Kutoa elimu ya afya bora na mazingira sehemu za kazi.
- Kuimarisha Bima za Afya sehemu zote.
- Kutekeleza Mikataba ya ILO.

## MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA AFYA NA USALAMA KAZINI

- Ukaguzi wa afya za wafanyakazi na utoaji wa huduma ya afya sehemu za kazi.
- Uwekaji wa mazingira safi na salama kazini, ukaguzi wa mitambo, mashine na vitendea kazi.
- Upatikanaji wa vifaa vya kinga na uwajibikaji katika masuala ya usalama kwa kila muajiri na mwajiriwa.

- Elimu kwa wafanyakazi juu ya afya na usalama kazini.
- Usimamizi mzuri wa mwajiri na ushirikishwaji wa mfanyakazi katika masuala ya afya na usalama kazini.

## ZATU YAFANYA UCHAGUZI

Chama cha Walimu Zanzibar (ZATU) kimefanya uchaguzi kwa ngazi ya Skuli / taasisi, tawi, kanda na taifa.
Uchaguzi wa ngazi ya skuli/taasisi uliwachagua wawaskilishi wa skuli /taasisi. Uchaguzi wa tawi uliwachagua Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe Watano wa Kamati Tendaji ya Tawi na Wajumbe Kumi wa Mkutano Mkuu wa Kanda.
Uchaguzi wa ngazi ya kanda uliwachagua Mwenyekiti, Wajumbe Sita wa Bazara Kuu Taifa, Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Kanda na Wajumbe Ishirini wa Mkutano Mkuu Taifa.

Uchaguzi ngazi ya Taifa uliwachagua Rais, Makamo wa Rais, Wajumbe Saba wa Kamati Tendaji Taifa, Wajumbe Watano wa Mkutano Mkuu Shirikisho na Wajumbe Watano wa Baraza Kuu Shirikisho. Chaguzi hizo zilitanguliwa na Mikutano Mikuu ya ngazi mbali mbali.

Akifungua Mkutano Mkuu Taifa Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi alisema hatua ya kufanya uchaguzi ni kudhihirisha dhana ya utawala bora, hivyo amewataka wajumbe wa mkutano huo kuhakikisha wanachagua viongozi bora watakaokiongoza Chama cha Walimu Zanzibar ili kuleta manufaa zaidi kwa walimu na taifa kiujumla. Aidha, Rais Dkt. Mwinyi aliwaomba walimu ambao hawajajiunga na ZATU kujiunga katika chama hicho.

Katika mkutano huo wageni mbalimbali walialikwa wakiwemo viongozi wa vyama vya walimu kutoka Kenya, Uganda, Burundi na Denmark.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Mhe. Lela Muhamed Mussa amewataka walimu kuunga mkono jitihada za Dkt. Mwinyi kwa kuipa kipaumbele sekta ya elimu na kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta hiyo.

Kwa upande wake Rais wa ZATU, mwalim Seif Mohammed Seif ameishukuru WEMA kwa uhusiano mzuri walionao wa masuala mbali mbali ya maendeleo ya elimu nchini.

Mikutano mengine ilikuwa ni Mkutano Mkuu wa Kanda ya Unguja na Pemba. Katika mikutano yote mikuu ziliwasilishwa taarifa za utekelezaji wa mipango kazi ya ZATU kwa kipindi cha 2018-2023.




Rais wa Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu CCM, Waziri wa Elimu , Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba katika picha ya pamoja na Rais wa ZATU, wakiimba wimbo wa mshikamano wa wafanyakazi




Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Nane ZATU Taifa wakiwa katika zoezi la upigaji kura.

Viongozi waliochaguliwa katika Mkutano Mkuu wa Nane ZATU Taifa ni hawa wafuatao.

1. Rais wa ZATU — Mwl. Seif M.Seif
2. Makamo wa Rais wa ZATU — Mwl. Khadija S. Kassim
3. Wajumbe Saba wa Kamati Tendaji Taifa
   - i. Mwl. Abeida Adi Seif
   - ii. Mwl. Ali Makame Tani
   - iii. Mwl. Fathiya Abeid Iddi
   - iv. Mwl. Fatma Ali Buda
   - v. Mwl. Said Mussa Abdalla
   - vi. Mwl. Omar Khamis Hamad
   - vii. Mwl. Sheha Ali Khamis
4. Wajume Watano wa Baraza Kuu Shirikisho
   - i.Mwl. Khamis Haji Ali
   - ii. Mwl. Suleiman Salum Abdalla
   - iii. Mwl. Abdulhamid Ali Vuai
   - iv. Mwl. Biubwa Massoud Abdalla
   - v.Mwl. Amini Amran Yunus
5. Wajumbe watano wa Mkutano Mkuu shirikisho
   - i.Mwl. Safia Said Massoud
   - ii.Mwl. Juma Khamis Juma
   - iii. Mwl. Massoud Othman Bakar
   - iv. Mwl. Rehema Simai Jecha
   - v. Mwl. Halima Ali Salim

Katika kukamilisha safu ya uongozi ZATU imefanya uteuzi wa viongozi wafuatao:

| | |
|---|---|
| 1. Katibu Mkuu | Mwl. Haji J. Omar |
| 2. Naibu Katibu Mkuu | Mwl. Salim A. Salim |
| 3. Mtunza Hazina | Mwl. Badi Kh. Moh'd |
| 4. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa | Mwl. Zuwena I. Wakil |
| 5. Mwenyikiti wa Kamati ya Walimu Wakuu Taifa | Mwl. Khatib R. Mwinyi |
| 6. Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa | Mwl. Nassor K. Ali |
| 7. Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu Wenye Ulemavu Taifa | Mwl. Nadya M. Ame |
| 8. Wajumbe Wawili wa Bazara Kuu wa Kuteuliwa (Unguja) | Mwl. Khadija J. Ali<br>Mwl. Mcha N. Foum |
| 9. Wajumbe Wawili wa Bazara Kuu wa Kuteuliwa (Pemba) | Mwl. Salama A. Bakari<br>Mwl. Faki O. Juma |
| 10. Mratibu wa Wanawake Kanda ya Unguja | Mwl. Salma Mb. Khatib |
| 11. Mratibu wa Wanawake Kanda ya Pemba | Mwl. Biubwa M. Abdalla |
| 12. Mratibu wa Walimu Wakuu Kanda ya Unguja | Mwl. Ghanima A. Abdalla |
| 13. Mratibu wa Walimu Wakuu Kanda ya Pemba | Mwl. Abdulrahman H. Bakar |
| 14. Mratibu wa Vijana Kanda ya Unguja | Mwl. Halima R. Khamis |
| 15. Mratibu wa Vijana Kanda ya Pemba | Mwl. Seif A. Hamad |
| 16.Mratibu wa Walimu Wenye Ulemavu Kanda ya Unguja | Mwl. Asha H. Awesu |
| 17.Mratibu wa Walimu Wenye Ulemavu Kanda ya Pemba | Mwl. Kai O. Haji |